Toleo 70 - Rabi' II 1444 H / Novemba 2022 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Chini ya Makucha ya Mfumo Muovu wa Kibepari Maisha Yanaendelea kuwa Magumu na Dhiki Zaidi

**HABARI NA MAONI**
Uingereza Yatangaza Kufilisika, Kwa Kukubali Kutawaliwa na "Watumwa" wa Miaka ya Jana

**MATOLEO**
Je, Maandamano ya Iran Yanaweza Kufanikiwa?

**JIBU LA SWALI**
Usahihi wa Hadith "Watakuja Watu Siku ya Kiyama, Imani yao itakuwa ya Kustaajabisha..."




## Uislamu dhidi ya Ajenda ya Kisekula ya LGBTQ

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

KUMB: 02/1444 Alhamisi, 24 Rabi'I 1444 H 20/10/2022 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Chini ya Makucha ya Mfumo Muovu wa Kibepari Maisha Yanaendelea kuwa Magumu na Dhiki Zaidi

Gharama za maisha nchini zinaendelea kuwa juu zaidi kwa kupanda maradufu bei za vyakula na bidhaa nyengine hali inayowafanya raia wa kawaida wakaukiwe mifukoni na kuwaacha kutapatapa wasijue nini cha kufanya! Wakenya wanaitaka na kuiomba serikali iliyoko mamlakani kwa sasa itatue tatizo hili ambalo ndani ya mfumo wa kibepari limekuwa ni dimbwi la kudumu.

Sisi katika Hizb ut Tahrir tungependa kusisitiza yafuatayo:

Utawala ulioko sasa kattu hautotatua tatizo hili kimsingi ambalo limekuwa ni kero ya mara kwa mara kwenye tawala za kibepari. Ukweli ukibakia kuwa sera za kiuchumi zinazotokamana na mfumo wa kiuchumi wa kibepari zilizoainisha bei kuwa ndio kigezo kikubwa cha uzalishaji wa rasilimali, usambazaji wake na matumizi ya bidhaa na huduma hivyo kupelekea kuweko kwa mashirika ya watu binafsi wanaomiliki soko peke yao kwa lengo la kujiongezea faida maradufu kwa gharama za mwananchi wa kawaida. Fauka ya haya, kihakika tawala za kibepari kimsingi ndio zinazostahiki kubebeshwa lawama kwa hali hii ngumu ya kiuchumi kwani zimeegemea mfumo uliofeli wa kiuchumi, kwa maana hii dhana ya kuwa utawala huu ulioko ni msafi wa kutofanya makosa yaleyale yaliyofanywa na tawala zilizopita ni jaribio lake la kuficha kufeli kwa mfumo wa kibepari.

Katika Uislamu ushibishwaji wa mahitaji msingi na uwezashaji wa kuyafikia mahitaji ya ziada yote ni jukumu linaloangukia serikali. Na kwa kigezo hiki Khalifah huwajibishwa kuliacha soko kuwa huru yaani kutoingiliwa na genge maalumu la wafanyibiashara walafi na wanasiasa wa choyo. Hatua hii itafanya soko kimaumbile lijipeleke kwa nishati ya mahitaji na usambazaji hivyo kufanya bei za bidhaa zenye ushindani na nafuu. Isitoshe, Uislamu umetatua tatizo la kiuchumi kwa msingi ya usambazaji wa utajiri (rasilimali) wala sio kama Urasilimali unavyosema kuwa tatizo la kiuchumi ni kupitia uzalishaji.

Kama ilivyoshuhudiwa katika historia ya Ukhalifa wa Umar ibn Al-Khattab (Khalifah wa pili wa Dola ya Kiislamu), wakati watu wa jimbo la Hijaz walipokumbwa na njaa kali, alitekeleza sera ya kiuchumi iliohakikisha kwamba hakuna mtu au kikundi chochote kinachoweza kuhujumu soko kwa kutaka kujichukulia faida na mtaji kwa kudhuru watu wakati wa ukame huo. Alichofanya Bin Khattab RA alitoa amri ya kiutendaji kwa Amr bin Al-As wakati huo gavana wa Afrika Kaskazini kuongeza usambazaji wa chakula katika soko la Madinah ili kupunguza bei ya juu na njaa.

Tunathibitisha kwamba kwa kuasimamishwa tena kwa Khilafah (Ukhalifa), migogoro na matatizo yote ya kiuchumi itatatatuliwa kwa ukamilifu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut-Tahrir Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Porojo za Vita Dhidi ya Ugaidi Zinaendelea

**Habari:**

Mnamo Jumatatu tarehe 19/09/2022 Tanzania iliungana na nchi nyingine za Afrika katika kutekeleza Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Afrika (AU) wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi. Baada ya kupitishwa azimio la kuridhiwa kwa itifaki hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Yusuph Masauni alisema kuwa Tanzania ina nafasi kubwa ya kupata manufaa kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao na kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia kuhusu ugaidi kupitia ushirikiano wa karibu kutoka kwa nchi wanachama.

**Maoni:**

Ni ukweli ulio wazi kwamba propaganda ya 'vita dhidi ya ugaidi' nchini Tanzania, mataifa ya Afrika na nchi zinazoendelea kwa ujumla ni mbinu ya kikoloni ya Wamagharibi ya kupambana na Uislamu, unyonyaji na uingiliaji wa mifumo ya usalama. Wakoloni Wamagharibi wanalazimisha mataifa dhaifu kuwaua, kuwatesa na kuwafunga watu wao wenyewe kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi kwa kubadilishana na hongo ya nchi za Magharibi inayoitwa fedha kwa ajili ya kupambana na ugaidi.

Nchini Tanzania haijawahi kutokea kesi ya wazi ya "gaidi" yeyote aliyekamatwa, licha ya propaganda za muda mrefu. Juni, 2019 aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Bwana Kangi Lugola alithibitisha kuwa hakuna tishio la ugaidi nchini Tanzania, kabla ya hapo Februari 2017 aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Harrison Mwakyembe aliliambia bunge kuwa hakuna taarifa yoyote ya tishio la ugaidi iliyoripotiwa nchini katika miaka ya hivi karibuni.

Taarifa zote hizi rasmi zinathibitisha ukweli mmoja, ambao ni kutokuwepo ugaidi wa kweli nchini badala yake kuna matumizi ya propaganda ya kimataifa ya vita dhidi ya ugaidi inayolenga Uislamu na Waislamu duniani kote na pia kuvuruga amani na maelewano na kurahisisha njia ya unyonyaji wa Wamagharibi kwa rasilimali za ulimwengu wa tatu.

Vyombo vya kusimamia sheria nchini Tanzania kwa muda mrefu vimekuwa vikitumia suala la ugaidi kutengeneza na kubambikia kesi dhidi ya Waislamu, wanaharakati na viongozi wao. Kesi hizi za kubambikiwa zimekuwa zikiisha kwa aibu ambapo jamhuri siku zote hushindwa kuleta ushahidi wowote kuthibitisha madai yao.

Zaidi ya hayo, kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi na visingizio vingine, wengi wameteseka mikononi mwa vyombo vya sheria ambavyo vimekuwa vikiwaua, kuwapora, kuwateka nyara, kuwaweka kizuizini kwa muda mrefu bila kufunguliwa mashtaka nk.

Kwa mfano, mwaka wa 2006, maafisa waandamizi wa jeshi la Polisi akiwemo SSP Christopher Bageni, waliwaua wafanyibiashara watatu wa madini na dereva wa teksi. Pia zaidi ya wahanga 380 hawajulikani waliko hadi leo kufuatia uvamizi wa serikali katika vijiji vya Mkuranga, Kibiti na Rufiji mwaka 2017, uvamizi ambao "haukufanyika kwa mujibu wa sheria na ulioambatana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mateso na mauaji ya kiholela" (The East African, Mei 05, 2018)

Bila ya kusahau kwamba mamia kama sio maelfu ya Waislamu na wengine waliwekwa kizuizini kwa miaka mingi bila kesi zao kusukilizwa, kama vile viongozi wa kikundi cha Uamsho kutoka Zanzibar waliowekwa kizuizini kwa takriban miaka minane na kufunguliwa mashtaka ya kubambikiwa yanayohusiana na ugaidi. Kisha serikali iliyabwaga mashtaka yao kwa aibu mwaka 2021. Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, alithibitisha kwa waandishi wa habari kufutwa kwa mashtaka yote. Hali kama hiyo iliwakuta wanachama watatu wa Hizb ut Tahrir Tanzania ambao walizuiliwa bila kesi yao kusikilizwa kwa zaidi ya miaka minne baada ya kushtakiwa kwa kesi ya kubambikiwa ya ugaidi, ambapo hatimaye waliachiliwa huru tarehe 22 Februari 2022, kufuatia DPP kuthibitisha kwamba hawana ushahidi wa kukinaisha kuendelea na mashtaka yanayodaiwa.

Pia, Mwenyekiti wa chama kikuu cha siasa cha upinzani (Chadema) nchini Tanzania, bwana Freeman Mbowe alikamatwa Julai 2021 katika uvamizi wa usiku jijini Mwanza, kabla ya mkutano wa hadhara wa kudai marekebisho ya katiba na kufunguliwa mashtaka yanayohusiana na ugaidi, kisha aliachiwa huru baada ya kukaa rumande kwa miezi saba.

Hiyo ni mifano michache tu kati ya mamia na maelfu ya watu waliowekwa kizuizini kwa kesi za kubambikiwa zinazohusiana na ugaidi ambapo 99.9% ni Waislamu ambao serikali imeshindwa kuthibitisha madai yao mbele ya mahakama hata baada ya miaka mingi ya kile kinachoitwa upelelezi. Hii ina maana kwamba hakuna hata mmoja wao aliyefanya vitendo vyovyote vya ugaidi, ndiyo maana jamhuri ilishindwa kuwasilisha ushahidi wowote thabiti dhidi yao.

Tunasisitiza tena kwamba, kampeni ya kupambana na ugaidi ni ajenda ya kigeni ya Kimagharibi na lazima ikomeshwe, kwa kuwa sheria na mikataba yake ni chombo cha kikatili cha kupambana hususan na Waislamu na Uislamu.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**

**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Uingereza Yatangaza Kufilisika, Kwa Kukubali Kutawaliwa na "Watumwa" wa Miaka ya Jana

**Habari:**

Rishi Sunak ametoa ombi la umoja katika kukabiliana na "changamoto kubwa ya kiuchumi," baada ya kushinda kinyang'anyiro cha kuwa waziri mkuu mpya. Alishinda kinyang'anyiro cha uongozi wa Tory baada ya mpinzani wake Penny Mordaunt kushindwa kupata uungwaji mkono wa kutosha kutoka kwa wabunge. Katika hotuba yake ya kwanza, Bw Sunak alisema kuleta chama chake na kwamba Uingereza kwa pamoja itakuwa "kipaumbele chake kikuu". Bw Sunak atakuwa waziri mkuu wa kwanza wa Uingereza wa asili ya Asia na mwenye umri mdogo zaidi kwa zaidi ya miaka 200. Bw Sunak - mwenye umri wa miaka 42 mshika dini ya Kibaniani - anatarajiwa kuchukua wadhifa huo mnamo Jumanne baada ya kuteuliwa rasmi na Mfalme. Anachukua nafasi ya Liz Truss, kufuatia kujiuzulu kwake kwa siku 45 tu katika uwaziri mkuu wake uliokumbwa na misukosuko wiki iliyopita. (BBC)

**Maoni:**

Yeyote anayefikiri kwamba 'Uingereza,' mama wa ukoloni na ubaguzi wa rangi, imekuwa nchi inayoheshimu ubwana wa nchi "zinazoendelea" na imeachana na ubaguzi wake wa rangi wa kuchukiza, baada ya kuanzisha himaya yake juu ya utumwa wa watu, haswa watu wa Bara Hindi, imekosea vibaya sana!

Badala yake, kinachoulazimu ufalme wa Uingereza kumkubali Muhindi kuingia katika jumba lao la klabu, ni kufilisika kwao kabisa kisiasa na kiuchumi. Kufilisika huku kulitokea baada ya Uingereza kupoteza ushawishi wake wa kikoloni katika maeneo mengi ya dunia, kuanzia Bara Hindi Dogo, kupita Mashariki ya Kati na kuishia Afrika. Kwa hiyo sababu ya kukubali kuingia kwa "watumwa" ndani ya jumba hilo inadhihirisha kiwango cha hasara kubwa iliyopatikana na jumba hilo. Hata hivyo, hasara hiyo kubwa haifidiwa kupitia kukubaliwa kwa "watumwa."

Hebu tuchukulie rundo kubwa la hasara ambayo Ulaya, ikiwemo Uingereza, imepata kutokana na vita vya Ukraine. Uingereza haiwezi kushindana tu na Amerika, au hata kutembea katika kivuli chake. Uingereza imekuwa nchi ya pambizoni. Uzito wake sio zaidi ya nchi yoyote ya Ulaya, ya kiwango cha pili au cha tatu. Haiwezi kushawishi hali ya kimataifa, au hata ile ya kanda ya Ulaya.

Kuchaguliwa kwa Sunak, na kukubaliwa kwake na ufalme wa Uingereza kama waziri mkuu, kunaendana na mabepari wabaguzi wa rangi nchini Marekani, kumruhusu Obama "mweusi" kuingia Ikulu ya White House. Inathibitisha kwamba watawala halisi, wa nchi zote mbili za kirasilimali za kikoloni, sio wale wanaokaa kwenye viti rasmi, ima ndani ya Ikulu ya White House au House of Commons. Badala yake, ni wamiliki halisi wa makampuni, na wamiliki wa mali na manufaa yaliyoporwa kutoka kwa wakoloni na nchi zilizokandamizwa duniani. Wanasiasa, weupe, weusi na Wahindi si chochote ila waajiriwa wa kusimamia nyadhifa rasmi nchini. Huu ndio uhalisia wa mfumo wa serikali katika nchi za Magharibi.

Marekani inajaribu kutopingika katika hali ya kimataifa, kwa kufanya kazi ya kuvunja mbavu za dubu la Kirusi nchini Ukraine, Ulaya inayoganda katika baridi kali na kumzimua panda wa Kichina. Inategemea kikamilifu vibaraka wake miongoni mwa watawala katika ulimwengu wa Kiislamu, kwa ajili ya kuunyenyekesha Umma wa Kiislamu. Dola za Kimsalaba za Ulimwengu wa Kale hazina uwezo tena, au hata kuwa tayari, kukabiliana na Umma wa Kiislamu, kama Ummah utapiga hatua kusimamisha dola ya Khilafah, sasa.

Siku hizi ni fursa ya dhahabu kwa wanyofu wote katika Ummah huu, na walio kileleni mwao ni Waislamu wanyofu miongoni mwa majeshi ya Waislamu. Ni lazima watoe Nusrah yao katika kunusuru Dini yao, wakiegemea upande wa Ummah wao. Ni lazima watoe Nusrah yao kwa Hizb ut Tahrir ili kusimamisha Dola ya Khilafah. Je, watapoteza fursa hii kwa Ummah na wao wenyewe? Je, watapoteza izza ya dunia na neema ya Akhera?! Au wataichukua fursa hii ya kuilinda Dini ya Mwenyezi Mungu (swt) na kheri ya umma, ili wapate izza ya dunia, radhi za Mwenyezi Mungu (swt), na neema ya Pepo?! Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

**(وَفِي ذَٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ الْمُتَنَافِسُونَ) "Na katika hayo washindanie wenye kushindana."** [Surah Al-Mutafifeen 83:26].

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bilal Al-Muhajir – Wilayah Pakistan**



Pepe: info@uqab.or.ke

# Afrika Yalazwa Njaa Kikatili Na Wakoloni Wa Kibepari Chini Ya Uangalizi Wa Viongozi Wake Wafisidifu

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Shaban Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

**Habari:**

Onyo la Mashirika ya FAO –WFP juu ya maeneo yanayokabiliwa na ukame kuhusu ripoti ya tahadhari ya mapema kuhusu uhaba wa chakula iliyotolewa na mashirika haya mawili ya kimataifa(Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) inatoa mwito wa kuchukuliwa hatua za haraka za kibinadamu ili kuokoa maisha na kuzuia njaa katika nchi zenye uhaba mkubwa wa chakula ambapo unatarajiwa kuwa mbaya zaidi kuanzia Oktoba 2022 hadi Januari 2023. Tayari katika eneo la Pembe ya Afrika, zaidi ya watu milioni 37 katika eneo hilo wanatarajiwa kufikia kiwango cha juu zaidi cha Kiwango cha Uainishaji cha Awamu ya Usalama wa Chakula (IPC3). )

**Maoni:**

Madhara ya ukame ni makubwa hasa maeneo ya mashariki na kusini mwa Ethiopia, mashariki na kaskazini mwa Kenya, na kusini na kati ya Somalia. Hii ina maana kwamba idadi kubwa ya watu iko katika hali mbaya, na ina uwezo mdogo wa kupata mahitaji ya kiwango cha chini ya chakula na hilo hufikiwa ima kwa kukatiza pakubwa zile bidhaa msingi au kwa kile kiitwacho mikakati ya kukabiliana na mgogoro.

Kwa miongo kadhaa,eneo la pembe ya Afrika bali bara lote limekabiliwa na majanga chini ya mnyororo wa ukoloni wa kibepari. Afrika imesibiwa na Mauaji ya halaiki, kuharibiwa kwa miundo mbinu, uporaji wa rasilimali,ukame na umasikini. Tawala za kibepari pamoja na mashirika ya kimataifa ya kutoa misaada yako mbali mno kuweza kufikia kwenye suluhisho la kweli juu ya majanga na maafa haya!

Sababu msingi hasa kwa nini watu wana njaa katika sehemu hii ya bara ambayo kiujumla haina mahusiano na uhaba wa mvua au mabadiliko ya hali ya hewa na migogoro kama inavyodaiwa na vyombo vya habari na taasisi za chakula na utafiti duniani; badala yake, inahusiana kwa pakubwa na sera mbovu za kiuchumi za mfumo wa Kibepari pamoja na tawala mbovu na wanasiasa ambao hawajali chochote isipokuwa matakwa yao ya uchoyo. Afrika ambayo inajumuisha sehemu ya pembe yake ina utajiri mkubwa wa asili yakiwemo madini, mito, ardhi kubwa yenye rutuba, lakini, rasilimali hizi zinatumiwa na mabwenyenye wa makampuni pekee wanaojinufaisha huku raia wakiishia mikono mitupu! Bara hili tajiri limenyanyaswa kinyama, na watu wake wanakufa njaa kikatili chini ya uangalizi wa viongozi wake. Hili limefafanuliwa vyema na mwandishi Torm Burgis katika kitabu chake ‘The Looting Machine’ ambapo anaeleza jinsi wingi wa malighafi unavyopelekea baadhi ya mabwenyenye wa Kiafrika, wafadhili wa nchi za Magharibi, waekezaji waovu Wachina, na hata Benki ya Dunia kupora na kunyonya Afrika.

Afrika kamwe haitoweza kujinasua na hali mbaya ila kwa kuyaondoa mashirika ya wamagharibi yanayonyakua na kufukarisha ardhi kuchimba lindi la umasikini,ujinga na maradhi. Njia ya Afrika kujitoa hakuna ila waachiliwe kulima ardhi zao zenye rutuba na kula mazao yake waachane kabisa na kuchukua suluhisho za mataifa ya kigeni ambayo ndiyo yanayofukarisha nchi na watu wake. Lakini hili nalo haliwezekani ispokuwa kwa kuangalia na kutatua tatizo la utawala na mfumo unaotakikana hapa duniani kutekelezwa.

Ni muhimu kufahamu kwamba ndwele hii inayokumba pembe ya Afrika yapaswa itie chachu Afrika kufanya kazi kwa haraka pamoja na harakati ya kiulimwengu ya Hizb ut-Tahrir kusimamisha utawala wa Khilafah chini ya mfumo wa Utume kwani pekee ndio utakaolinda Afrika na ulimwengu kwa ujumla dhidi ya majanga haya, kusitisha kabisa uingiliaji wa kikoloni katika ardhi zetu na hapa kuhakikishia kila raia ndani yake ya anapata usalama wa chakula.

Kwa ukumbusho, ni chini ya Khilafah ya Umar Ibn Khattab pindi Madina iligubikwa na baa la njaa akawaandikia Mawalii kuwataka wapeleke nafaka ya chakula Arabuni. Ngamia waliobea shehena ya nafaka ya chakula na mahitaji mengine yalikuja kutoka Syria, Iraqi, na Misri. Milo ilipikwa katika ngazi ya Jimbo na watu wote waliokimbilia Madina walilishwa kila siku kwa gharama za serikali. Kulingana na akaunti moja, watu takriban watu 40,000 walilishwa kila siku. Umar (ra) alikataa kula nyama au siagi wakati wa kipindi cha njaa. Tumbo lake lilikuwa likiunguruma, lakini akasema: “Ewe tumbo unaweza kunguruma upendavyo, lakini maadamu njaa inaendelea, siwezi kukuruhusu kitu chochote kitambo.”.

# Waislamu wa Dearborn, Michigan Wasimama Imara kwa ajili ya Ulinzi wa Watoto Wetu

## Uislamu dhidi ya Ajenda ya Kisekula ya LGBTQ

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَاراً وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ

**"Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa."** [At-Tahrim 66:6]

Macho yote yako kwa Dearborn, Michigan - nyumbani kwa mkusanyiko wa idadi kubwa zaidi ya Waarabu-Waamerika nchini - kama wazazi, haswa na wazazi Waislamu, kwa ujumla wakipinga usambazaji wa vitabu viovu vya LGBTQ katika mfumo wa shule za umma wa jiji hilo. Maandamano ambayo yalisonga na kufunga kumbi za bodi ya shule yalichemka huku jumuiya na bodi ya shule zikitofautiana, bodi ya shule ikilazimisha mamlaka ya Dola ya Kisekula dhidi ya jamii iliyohisi sauti zao, wasiwasi na mamlaka yao juu ya watoto wao yamenyakuliwa. Huu ni mvutano wa kawaida unaopasua mishipa ya nchi, huku makundi yanayoonekana kuwa ya wachache kama vile la ushawishi wa LGBTQ yakifurahia kuungwa mkono na mfumo huo dhidi ya jamii nyingi za kitamaduni zinazoonekana kuwa kimya—hata hivyo, ya kwanza inayoonekana nchini Marekani ni jamii ya Waislamu. Ishara moja iliyoshikiliwa katika maandamano hayo, haswa, ilinasa mfadhaiko uliopo, ikisema kwamba "Ikiwa Demokrasia Ni Muhimu, Sisi ndio Wengi."




Uhalisia ulio nyuma ya mfadhaiko huu – ni haki za nani, sauti ya nani, na mfumo wa nani wa maisha ambao kikweli ndio unao stahiki - yanaingia ndani zaidi kuliko mfululizo wa matukio yanayotokea huko Dearborn, Michigan, na yanazungumzia mfumo usiofungamana, unaogongana, na wenye upendeleo wa Demokrasia ya Kisekula yenyewe. Katika kuondolewa kwa Mungu kutoka kwa nyanja ya maisha ya umma na ya kijamii, hakuna chanzo cha maadili yenye malengo, sahihi au batili, na badala yake hushindana vyama mbalimbali kwa maslahi yao binafsi - mara nyingi kwa gharama ya wale walio dhaifu kinguvu au kiidadi. Pasi na majibu sahihi, jibu pekee lililobaki ni kwamba linaweza kufanya sawa! Si ajabu kwamba Dola ya Kisekula inaposonga mbele, badala ya utulivu na mshikamano, kinachozuka ni sauti zinazopingana, siasa za upendeleo, kuchanganyikiwa, na vurugu. Leo watoto wanaweza kutafuta tiba ya kuzuia homoni na upasuaji usioweza kutenduliwa bila hata idhini ya wazazi wao, muundo wa kawaida wa familia una changamoto, na daima kuna alfabeti inayoongezeka kila wakati ya kitambulisho kipya cha kijinsia na uhalisia unaolazimishwa juu ya watu.

Uislamu, kinyume chake, ni mfumo kamili wa maisha, nidhamu, na muundo ambao uko wazi kabisa, bila mgongano, na ndio tiba pekee ya hali ya Kijahiliyah (ujinga, dhulma, kuchanganyikiwa, hali kupotea) leo. Uislamu ni sahali, uliofupishwa katika uthibitisho wake wa imani: kwamba hapana Mungu wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad (saw) ndiye Mtume wa mwisho wa Mwenyezi Mungu – na kwamba kila kinachotokana na hayo ni haki, sahihi kimaadili, na msingi ambao kwao mujtamaa hujengwa. Uhalisia hivi leo ni kwamba mifumo mingine yote ya maisha imeinama, imefungana, au imelegea kuhusiana na Mfumo wa Kilimwengu wa Kisekula - yaani, isipokuwa Uislamu! Kwa hiyo, kama Waislamu, tuna wajibu wa kushikamana, kusimama kidete, na kuwalingania wengine kwa yale ambayo ni bora kwao katika maisha haya na yajayo. Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw) wametangaza yale yanayostahiki na yasiyostahiki katika suala la muundo wa familia, mahusiano ya kijinsia, sahihi na makosa – na jibu la Muislamu aliyeukubali msingi huo ni kusema tu kwa kujibu kwamba tunasikia, na tunatii - bila kujali shinikizo, siasa ndogo ndogo za upendeleo, au bodi ya shule!

*Endelea... UK 7*



Pepe: info@uqab.or.ke

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا

**“Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi.”** [Al-Ahzab 33:36]

Kwa kumalizia, ni jambo la kutia moyo sana kuona jamii ya Waislamu huko Dearborn ikisimama kulinda usafi wa watoto wetu. Waislamu kote nchini tunatakiwa kuwaunga mkono wazazi na watoto wenzetu. Kwa kufanya hivyo lazima tufanye yafuatayo:

1. Wazazi wanapaswa kupambana na maadili ya kiliberali ya Kisekula kuanzia umri mdogo sana na kuwashajiisha watoto kufikiri kwa kina juu ya kile wanachofundishwa na kupinga fikra hizi kwa fikra wazi za Kiislamu.

2. Tambua kwamba shule na jamii kwa jumla huwafunza watoto fikra na maadili ya kiliberali ya kisekula. Kwa hivyo, ni muhimu sana kueleza msimamo wa Kiislamu juu ya uhusiano wa mwanamume na mwanamke, ndoa, uhusiano wa kimwili, familia, mujtamaa na serikali. Ni lazima tuwafahamishe watoto mfumo wa kijamii wa Uislamu. Kwa kuongeza, hii inamaanisha kuelezea mfumo mbadala wa maisha kinyume na mfumo wa kiliberali wa kisekula.

3. Jamii ya Kiislamu lazima idai mashirika, viongozi na wanaharakati wa Kiislamu kujitenga na ajenda za Kiliberali (Democrat) au za mrengo wa Kulia (Republican). Lazima tupange mustakabali wetu wenyewe kulingana na Aqidah yetu ya kipekee, mawazo msingi na maadili bora.

4. Hatimaye, kujivunia Uislamu na maadili yetu na kuwalinda watoto wetu bila kujali ni majina gani ambayo wale wanaochukia haki wanaweza kutupa.

Familia zetu, majirani zetu, ardhi, na Ulimwengu wa leo wanahitaji sana rehma, utulivu, uadilifu na haki ya Uislamu—na kwa hiyo, umefika wakati sasa wa sisi kama jamii na Umma tufanye kazi na kuendesha harakati zetu kipekee chini ya bendera ya Uislamu na kwamba turegeshe tena sifa yetu kama Umma bora uliotolewa kwa ajili ya Wanadamu!

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُم مِّنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingeli kuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu”.** [Aal-i-Imran 3:110]

**H. 21 Rabi' I 1444**<br>**M. : Jumatatu, 17 Oktoba 2022**

**Hizb-ut-Tahrir**<br>**Amerika**



**Pepe: info@uqab.or.ke**

# Je, Maandamano ya Iran Yanaweza Kufanikiwa?



Maandamano nchini Iran sasa yamekuwa yakiendelea kwa zaidi ya mwezi mmoja nchini Iran tangu kifo cha Mahsa Amini mikononi mwa polisi wa maadili wa Iran, alipokamatwa kwa kukiuka kanuni za mavazi za nchi hiyo. Maandamano hayo yaliyotokea ni makubwa zaidi utawala huo wa watu wa dini kuwahi kukabiliana nayo kwa muda mrefu. Utawala huo wa watu wa dini umekuwa madarakani tangu Mapinduzi ya 1979, lakini miongo kadhaa ya ufisadi, uzembe na usimamizi mbovu wa kiuchumi utawala huo leo ni dhaifu kuliko ulivyowahi kuwa. Ingawa hakuna uwezekano wa serikali hiyo kupinduliwa, hakuna uwezekano pia kuwa inaweza kubakia hali katika muundo wake wa sasa bila kubadilika.

Wakati Shah alipopinduliwa mnamo 1979 simulizi ya utawala wa watu wa dini ilikuwa ni kufanyika kwa mapinduzi ya Kiislamu, ambayo yalikuwa dhidi ya Marekani, yote yalifanywa pamoja na Ayatollah Ruhollah Khomeini mwenye fikra huru, akiwa na malengo makubwa ya kuigeuza Iran kuwa dola ya kikanda. Licha ya mapinduzi hayo kuchukuliwa kuwa ya Kiislamu, makundi yaliyohusika zaidi yalikuwa yasiyo ya Kiislamu na yalijumuisha wakomunisti, wasomi, watu wa mrengo wa kushoto, vyama vya wafanyikazi na wengine wengi ambao hawakuwa wakitafuta mapinduzi ya Kiislamu. Akiwa madarakani Khomeini alijikita katika kukabiliana na vitisho vyote vinavyoweza kujitokeza kwa utawala huo mpya, jambo ambalo lilimpelekea kuyageuka makundi yote yaliyomsaidia kuingia madarakani. Khomeini alikuwa hofu sana hivi kwamba aliunda Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu (IRGC) kwani hakuliamini jeshi.

Utawala huo wa watu wa dini uliunda nguzo nyingi na taasisi za serikali kudumisha kushikilia kwao madaraka. Waliunda mfumo wa kisiasa ambao umewaruhusu kuitawala Iran na siasa zake tangu wakati huo. Kileleni mwa mfumo huu ni mtu mwenye nguvu zaidi, kiongozi mkuu, wadhifa ambao hadi sasa umeshikiliwa na watu wawili pekee. Wa kwanza alikuwa mwanzilishi wa jamhuri hiyo ya Kiislamu, Ayatollah Khomeini, ambaye alishikilia wadhifa huo kuanzia mwaka 1979 hadi kifo chake mwaka 1989. Alirithiwa na msaidizi wake mkuu na rais wa zamani wa awamu mbili, Ayatollah Ali Khamenei, ambaye amekuwa kiongozi mkuu wa nchi hiyo kwa miongo mitatu iliyopita na kwa sasa bado yuko mamlakani. Kiongozi mkuu hachaguliwi kwa kura ya umma bali na Bunge la Wataalamu, ambalo ni kundi la viongozi wakuu wa kidini. Ana mamlaka makubwa na huteua uongozi wa taasisi zenye nguvu zaidi za kisiasa za nchi hiyo, ikiwemo utangazaji wa serikali, Wanajeshi, Mkuu wa Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu (IRGC) na Baraza la Walinzi.

*Endelea... UK 9*

Utawala huo wa watu wa dini mithili ya utawala wa kinasaba wa Pahlavi kabla yake ulianzisha mfumo wa serikali kuu kwani ni 50% -60% pekee ya idadi ya watu wa Iran ndio Wafursi. Iran imegawanywa katika idadi kubwa ya makabila na utawala huo wa watu wa dini kama vile utawala kabla yake hudumisha hali ya usalama sio tu kudumisha utawala wake lakini pia kuwatawala watu walio wachache ambao wanaweza kuwa tishio. Kaskazini-Magharibi mwa Iran wanaishi kabila la Wakurdi na Waazheri ambao hawajioni kama Wafursi. Waazheri wana mavuguvugu ya kujitenga katika mkoa wa Ardabil na wanataka kujiunga na Azerbaijan. Kifo cha Mahsa Amini, ambaye alikuwa Mkurdi, kilisababisha eneo hili kufanya maandamano makubwa zaidi dhidi ya utawala huo. Wakurdi na Waazheri kwa muda mrefu wamekuwa wakitendewa vibaya na serikali kwani hawawaamini. Kusini-Magharibi ni eneo la kimkakati zaidi la Iran la Khuzestan ambalo linashikilia rasilimali zake za kawi. Hapa ndipo Waarabu walipokaa kwa muda mrefu, ambao wamechukua tofauti kwamba eneo hilo liliitwa Ahwaz na hii ilibadilishwa na serikali kuwa Khuzestan ili kuifanya iwe Kifursi. Utawala huo kwa muda mrefu umenyonya utajiri wa nishati wa maeneo hayo na kuacha fujo kubwa katika suala la umaskini na ukosefu wa ajira katika eneo hilo. Katika mipaka ya Mashariki ya Iran kwa muda mrefu kumekuwa na masuala kwenye mpaka wa Afghanistan na mkoa wa Sistan-Baluchistan, ambao idadi kikubwa ni Wasunni na daima umekuwa ukiyumba kwani watu wa huko wamehangaika na umaskini, huku utawala ukiwaona kama jamii inayoshukiwa. Iran ni taifa kubwa lenye nyanda na milima inayoweza kukaliwa na watu iliyozungukwa na maeneo ya vijijini na mijini ya Uajemi. Haya basi yamezungukwa na idadi kubwa ya makabila ya wachache na kwa pamoja wanalingana na idadi ya Wafursi.

Utawala wa watu wa dini umekabiliwa na maasi na maandamano mengi katika kipindi chote cha utawala wake wa miongo minne. Tunachokiona nchini Iran leo ni sura ya hivi punde zaidi ya hili. Mwanasosholojia mashuhuri wa Iran Mohammad Fazeli kutoka chuo kikuu cha Tehran alisema kuwa maandamano hayo si matokeo ya matukio ya hivi karibuni tu, bali ni zao la zaidi ya miaka 40 ya utawala mbaya nchini Iran. Fazeli alisema kuwa kuna matatizo mengi ambayo hayajatatuliwa ambayo yamekuwa yakiongezeka katika miongo minne iliyopita, bila ya jaribio lolote la serikali kuyashughulikia. Alisema, "Rais Raisi anaposema atachunguza kifo cha Mahsa Amini, watu hawawezi kumwamini kwa sababu kesi kama hizo hapo awali hazijatatuliwa." Wakati huo huo, kukosekana kwa matumaini ya siku za usoni baada ya miongo kadhaa ya mfumko mkubwa wa bei, ukuaji uliodumaa wa uchumi, kuzorota kwa mfumo wa utawala na mambo mengine mengi yamesababisha hasira dhidi ya utawala wa Iran, na Wairan wengi hawana tena hofu ya kuandamana na kuzungumza wazi dhidi ya utawala uliofeli wa watu wa dini.


Kilichowageuza wengi dhidi ya utawala wa watu wa dini ni ukweli kwamba baada ya miongo minne umeharibu uchumi, umefukarisha wananchi na unaendelea kuwakandamiza. Pato la Taifa la Iran lilipungua kwa 70% kutoka $599 bilioni mwaka 2012 hadi $191 bilioni leo! Viwango vya maisha nchini Iran leo vimefikia kiwango cha chini kabisa kwa zaidi ya karne moja. Bei zinaendelea kupanda, na kufanya bidhaa muhimu kama vile chakula na dawa, zisiweze kumudu Wairan wengi.

Nchini Iran mabadiliko ya kihistoria yamekuja kwa njia mbili. Ime serikali ya kigeni inavamia au kuunga mkono kikundi ndani ya Iran, hii ndio ilifanyika wakati Urusi na Uingereza ziliivamia Iran mwanzoni mwa WW1 na WW2 ili kuhakikisha inaweza kutumia rasilimali za nishati za Iran kwa juhudi za vita. Mnamo mwaka wa 1979 Wafursi na watu walio wachache na watu kutoka matabaka tofauti ya jamii walikusanyika ili kumpindua Shah. Leo watu walio wachache nchini Iran watahitaji uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa Wafursi ikiwa wanataka kuung'oa utawala huo. Harakati za upinzani kwa sasa zinafanya maandamano makubwa lakini zimegawanyika kwani hazina kiongozi mkuu na hazijahamasisha maeneo ya vijijini ambayo ndio ngome ya watu hao wa dini.

Hatua kwa hatua Iran inabadilika kutoka kwa dola ya kitheokrasi inayotawaliwa na watu wa dini hadi kuwa na serikali ya IRGC wanayojiona kuwa walezi wa mapinduzi ya 1979. Huku watu wa dini wakipoteza uaminifu, hakuna uwezekano baada ya kifo cha Khamenei, IRGC itahitaji kiongozi mkuu ili waendelee kubaki madarakani hivyo huenda kuwe na kiongozi mkuu mwenye uwezo mdogo kama nembo tu. Serikali ya kiimla inayoongozwa na kiongozi wa kijeshi huenda iwe ndio mustakabali wa Iran. Kama ile ile ya Iran mwanzoni mwa karne ya 20 wakati Kanali Reza Khan, alipokuwa waziri mkuu mwaka 1921, alimpindua Ahmad Shah mwaka 1925 na kuanzisha Utawala wa Nasaba wa Pahlavi.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Adnan Khan**




**Swali:**

Assalamu alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu

Mwenyezi Mungu akubali utiifu wako na heri ya mwaka mpya, Sheikh.

Nilikuwa nikitafuta usahihi wa Hadith hii, lakini sikuweza kupata usahihi ulio kwa maneno haya, kwa hivyo tafadhali nisaidie.

(Siku ya Kiyama, watakuja watu imani yao itakuwa ya kustaajabisha, nuru yao itatoka mikononi mwao na mikononi mwao ya kulia, na itasemwa: Leo mnafurahi, na amani iwe juu yenu ingieni humo milele, Malaika na Manabii watawaonea wivu kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwao. Basi, maswahaba wakauliza ni kina nani hao ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: si katika sisi wala si katika nyinyi, kwani nyinyi ni maswahaba zangu na hao ni vipenzi vyangu. Watakuja baada yenu na kukuta kitabu ambacho watu wameacha kukifuata na Sunnah waliyoiua, basi watakigeukia Kitabu na Sunnah na kuzihuisha na kuzisoma na kuzifundisha kwa watu, na watakumbana katika njia yake na adhabu kali zaidi kuliko mliyoyakabili. Imani ya mmoja wao ni kama arobaini katika nyinyi, na kuuawa shahidi mmoja wao ni kama arobaini katika mashahidi wenu. Mtapata wakuinusuru haki, lakini hao hawatapata wa kuwanusuru, wamezungukwa na wadhalimu kutoka kila mahali, na wako katika maeneo ya Bayt Al-Maqdis.” Na Mwenyezi Mungu akubariki.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam wa Rahmatullah wa Barakatahu

1- Kuhusu andiko (hadith) ambalo unauliza kulihusu, hatukulipata kwa maneno haya katika kitabu chochote cha Hadith, na inaonekana kwamba baadhi ya maneno yake yamechukuliwa kutoka katika Hadith kadhaa zilizounganishwa pamoja, kwa hivyo yeyote aliyefanya hivyo alizifanya zionekane kama Hadith moja:

1. Hadith zinazokusudiwa ni Hadith katika sura nyingi, na sio riwaya nyingi kwa Hadith moja.
2. Pia, baadhi ya Hadith zina maneno yanayokaribiana na yale yaliyotajwa katika matni (andiko) na sio maneno yale yale.
3. Katika andiko lililotajwa, pia kuna baadhi ya maana zilizotajwa katika baadhi ya Hadith ingawa maneno ni tofauti.
4. Zaidi ya hayo, miongoni mwa Hadith ambazo baadhi ya maumbo na maneno yalichukuliwa matni (andiko) husika, baadhi ni Hadith zinazokubalika ambazo hutumika, na baadhi si sahihi na hazitumiki kama dalili.

2- Nitataja baadhi ya zile Hadith zilizokubaliwa ambazo hutumika kama dalili:

- Ahmad amepokea katika Musnad yake kutoka kwa Abu Malik Al-Ash’ari kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alipomaliza swala yake, aliwageukia watu kwa uso wake na kusema:

*Endelea... UK 11*

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اسْمَعُوا وَاعْقِلُوا وَاعْلَمُوا أَنَّ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ عِبَاداً لَيْسُوا بِأَنْبِيَاءَ وَلَا شُهَدَاءَ يَغْبِطُهُمُ الْأَنْبِيَاءُ وَالشُّهَدَاءُ عَلَى مَجَالِسِهِمْ وَقُرْبِهِمْ مِنَ اللَّهِ

**"Enyi watu, sikilizeni, mutafakari, na mujue kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ana waja ambao si manabii, wala mashahidi, manabii na mashahidi wanawaonea wivu kwa ajili ya mikusanyiko yao na kujikurubisha kwao kwa Mwenyezi Mungu".** Basi akaja mtu mmoja katika wapokezi wa Mabedui na akampungia mkono Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na kusema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, watu ambao si katika manabii, wala mashahidi wa manabii, na manabii na mashahidi wanawaonea wivu kwa ajili ya mikusanyiko yao na kujikurubisha kwao kwa Mwenyezi Mungu, basi tusifie kuhusu wao. Basi, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akafurahishwa na swali la Bedui, hivyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akasema:

«هُمْ نَاسٌ مِنْ أَفْنَاءِ النَّاسِ وَنَوَازِعِ الْقَبَائِلِ لَمْ تَصِلْ بَيْنَهُمْ أَرْحَامٌ مُتَقَارِبَةٌ تَحَابُّوا فِي اللَّهِ وَتَصَافَوْا يَضَعُ اللَّهُ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مَنَابِرَ مِنْ نُورٍ فَيُجْلِسُهُمْ عَلَيْهَا فَيَجْعَلُ وُجُوهَهُمْ نُوراً وَثِيَابَهُمْ نُوراً يَفْزَعُ النَّاسُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يَفْزَعُونَ وَهُمْ أَوْلِيَاءُ اللَّهِ الَّذِينَ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ»

**"Hao ni watu kutoka katika maangamizo ya watu na fitina za makabila, wasio na mafungamano ya karibu ya kizazi baina yao, na waliopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atawawekea mimbari za nuru, na atawaketisha juu yake, na atazifanya nyuso zao kuwa nuru, na nguo zao kuwa nuru. Watu watakuwa na hofu Siku ya Kiyama, wala wao hawatatishika, na wao ni wandani wa Mwenyezi Mungu, ambao hawatakuwa na hofu, wala hawatahuzunika."**

- Muslim amepokea katika Sahih yake kutoka kwa Abu Hurairah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuja makaburini na kusema: السَّلَامُ عَلَيْكُمْ دَارَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ وَإِنَّا إِنْ شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لَاحِقُونَ وَدِدْتُ أَنَّا قَدْ رَأَيْنَا إِخْوَانَنَا **"Amani iwe juu yenu enyi nyumba ya waumini, na hakika sisi inshaAllah tutajiunga nanyi. Tunatamani lau tungewaona ndugu zetu".** Wao (wasikilizaji) wakasema: Je, sisi si ndugu zako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: أَنْتُمْ أَصْحَابِي وَإِخْوَانُنَا الَّذِينَ لَمْ يَأْتُوا بَعْدُ **"Nyinyi ni maswahaba zangu, na ndugu zetu ni wale ambao, bado hawaja duniani."** Wakasema: Wajuaje yule ambaye bado hajaja kutoka kwa Umma wako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu,? Akasema: أَرَأَيْتَ لَوْ أَنَّ رَجُلًا لَهُ خَيْلٌ غُرٌّ مُحَجَّلَةٌ بَيْنَ ظَهْرَيْ خَيْلٍ دُهْمٍ بُهْمٍ أَلَا يَعْرِفُ خَيْلَهُ **"Waonaje; lau mtu ana farasi ambao mgongoni mwao kuna mapaku meupe na meusi, je ataweza kuwatambua farasi wake?".** Wakasema: Ndio, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema:

فَإِنَّهُمْ يَأْتُونَ غُرّاً مُحَجَّلِينَ مِنَ الْوُضُوءِ وَأَنَا فَرَطُهُمْ عَلَى الْحَوْضِ أَلَا لَيُذَادَنَّ رِجَالٌ عَنْ حَوْضِي كَمَا يُذَادُ الْبَعِيرُ الضَّالُّ أُنَادِيهِمْ أَلَا هَلُمَّ فَيُقَالُ إِنَّهُمْ قَدْ بَدَّلُوا بَعْدَكَ فَأَقُولُ سُحْقاً سُحْقاً

**"Hakika wao watakuja Siku ya Kiyama wakiwa na nyuso, mikono, na miguu yao inang'aa, kwa sababu ya udhu." Kisha akasema: "Nami nitafika kwenye birika (al-hawdh) mbele yenu." Kisha akasema: "Watu watafurushwa kutoka kwa birika hilo, kama wanavyofurushwa ngamia waliopotea. Na nitawaita: "Njooni hapa!" lakini itasemwa: walibadilisha baada yako." Basi nitasema: "ondokeni ondokeni!"**

- Muslim amepokea katika Sahih yake kutoka kwa Uqbah aliyesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema: لَا تَزَالُ عِصَابَةٌ مِنْ أُمَّتِي يُقَاتِلُونَ عَلَى أَمْرِ اللَّهِ قَاهِرِينَ لِعَدُوِّهِمْ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَالَفَهُمْ حَتَّى تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ وَهُمْ عَلَى ذَلِكَ **"Kundi la umma wangu litaendelea kupigana kwa ajili ya amri ya Mwenyezi Mungu kwa kumtiisha adui yao, na wale wanaowapinga hawatawadhuru mpaka iwafikie Saa ya Kiyama wakiwa katika hali hiyo".**

- Ahmad amepokea katika Musnad yake kutoka kwa Al-Baraa bin Azib kwamba Mtume (saw) alimpiga mawe Yahudi mmoja (kwa kuzini) na akasema: اللَّهُمَّ إِنِّي أُشْهِدُكَ أَنِّي أَوَّلُ مَنْ أَحْيَا سُنَّةً قَدْ أَمَاتُوهَا **"Ewe Mwenyezi Mungu, nashuhudia kwako kwamba mimi ndiye mtu wa kwanza kuhuisha Sunnah ambayo walikuwa wameiua".**

- Ahmad amepokea katika Musnad kutoka kwa Abu Umamah aliyesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي عَلَى الْحَقِّ ظَاهِرِينَ لَعَدُوِّهِمْ قَاهِرِينَ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَالَفَهُمْ إِلَّا مَا أَصَابَهُمْ مِنْ لَأْوَاءَ حَتَّى يَأْتِيَهُمْ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَذَلِكَ قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ وَأَيْنَ هُمْ؟ قَالَ: بِبَيْتِ الْمَقْدِسِ وَأَكْنَافِ بَيْتِ الْمَقْدِسِ

**"Bado lingalipo kundi la Ummah wangu juu ya haki, linaloonekana kumshinda adui yao, na hawatadhurika na walio nyuma yao isipokuwa msiba utakapowafikia, mpaka iwafikie amri ya Mwenyezi Mungu hali wao wako hivyo. Wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wako wapi? Akasema: Katika Bayt Al-Maqdis na viunga vya Bayt Al-Maqdis".**

- Al-Tirmidhi amepokea katika kwa Sunan yake kutoka kwa Abu Umayyah al-Sha`bani ambaye amesema: Nilikwenda kwa Abu Tha'labah al-Khushni na kumwambia: unaamiliana vipi na Ayah hii? Akauliza: Aya ipi? Nikasema: Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا عَلَيْكُمْ أَنْفُسَكُمْ لَا يَضُرُّكُمْ مَنْ ضَلَّ إِذَا اهْتَدَيْتُمْ

**"Enyi mlio amini! Kilicho lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni walio potoka ikiwa nyinyi mmeongoka."** [Al-Ma'idah: 5-105] Akasema: Wallahi, Nilimuuliza mjuzi mmoja kuihusu. Nilimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na akasema:

«بَلِ ائْتَمِرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَتَنَاهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ حَتَّى إِذَا رَأَيْتَ شُحّاً مُطَاعاً وَهَوًى مُتَّبَعاً وَدُنْيَا مُؤْثَرَةً وَإِعْجَابَ كُلِّ ذِي رَأْيٍ بِرَأْيِهِ فَعَلَيْكَ بِخَاصَّةِ نَفْسِكَ وَدَعِ الْعَوَامَّ فَإِنَّ مِنْ وَرَائِكُمْ أَيَّاماً الصَّبْرُ فِيهِنَّ مِثْلُ الْقَبْضِ عَلَى الْجَمْرِ لِلْعَامِلِ فِيهِنَّ مِثْلُ أَجْرِ

*Endelea... UK 12*

خَمْسِينَ رَجُلاً يَعْمَلُونَ مِثْلَ عَمَلِكُمْ»

**“Amrisheni mema na katazeni maovu, hata mukiona ubakhili wa mtiifu na matamanio yanayofuatwa, na dunia yenye taathira na ajabu ya kila mwenye rai yake, huna budi kuwaacha watu wa kawaida. Kwani hakika nyuma yenu ni siku za subira, ndani yake ni kama kushika makaa ya moto, kwa yule afanyaye kazi ndani yazo ujira wake ni mithili ya ujira wa watu hamsini wafanyao kazi mithili ya kazi yenu”.** Abdullah bin Al-Mubarak amesema: “Mbali na Utbah kuniongezea kwamba ilisemwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ujira wa watu hamsini miongoni wetu au wao? Akasema: بَلْ أَجْرُ خَمْسِينَ مِنْكُمْ **“Bali ujira wa watu hamsini miongoni mwenu”.** Abu Issa amesema hii ni hasan lakini gharib.

3- Hadith zilizotajwa hapo juu ni Hadith zinazokubalika zinazumika. Lakini pia kulikuwa na Hadith ambazo ndani yake kulikuwa na ikhtilafu juu yake na zilikuwa na maneno na maumbo yanayofanana na matni inayozungumziwa, na nitataja baadhi yake ili kuonyesha kuwa matni inayozungumzwa imeundwa kwa Hadith kadhaa sahihi na zisizo sahihi.

Imekuja katika al-Ibana al-Kubra ya Ibn Battah kwamba Mtume (saw) amesema: رحمة الله على خلفائي **“Mwenyezi Mungu awarehemu watakaokuja baada yangu”,** wakasema: Wataokuja baada yako ni kina nani? Akasema: الذين يحيون سنتي، ويعلمونها عباد الله **“Wale ambao wanaihuisha Sunnah yangu na wanaifundisha kwa waja wa Mwenyezi Mungu”**, na imekuja katika Musnad ya Al-Shihab Al-Quda’i ya Katheer bin Abdullah Al-Muzni, kutoka kwa babake, kutoka kwa babu yake, aliyesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: إن الدين بدأ غريبا، وسيعود كما بدأ غريبا، فطوبى للغرباء **“Dini ilianza ikiwa ngeni, itarudi iwe ngeni kama ilivyo anza, basi bishara njema ni kwa wageni”,** Ikasemwa: ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao wageni ni kina nani? Akasema: الذين يحيون سنتي ويعلمونها عباد الله **“Wale ambao wanaihuisha sunnah yangu na wanaifundisha kwa waja wa Mwenyezi Mungu.”** Imeelezwa katika mkusanyiko wa hadith: اللهم ارحم خلفائي الذين يأتون من بعدي يروون أحاديثي وسنتي ويعلمونها الناس... **“Ewe Mwenyezi Mungu, warehemu watakaokuja baada yangu, watakaopokea hadith zangu na sunnah zangu na wakazifundisha kwa watu”** (Al-Tabarani katika Al-Awsat, Al-Ramhurmi katika Al-Muhaddith Al-Fasal, Al-Khatib katika Sharaf Al-Hadith, na Ibn Al-Najjar kutoka kwa Ibn Abbas kutoka kwa Ali Al-Tabarani amesema: Ahmad bin Issa Abu Taher Al-Alawi wakipekee. Amesema katika Al-Mizan: Al-Daraqutni amesema: msema urongo, na hivyo hadith hii ni batili. Ibn Abi Hatim, hakitaja jeraha au uzushi ndani yake), Al-Tabarani ameinakili katika Al-Awsat (6/77, Na. 5846). Al-Haythami (1/126) amesema: Inajumuisha Ahmad bin Issa Al-Hashimi.

Al-Daraqutni amesema: Yeye ni msema urongo. Na Al-Ramhorzi katika Al-Muhaddith Al-Fasal (1/163). Imesahihishwa pia na: Al-Dailami (1/479, Na. 1960). Al-Dhahabi amesema katika Al-Mizan (1/270, tafsiri 508) na Al-Hafiz amekuafikiana naye katika Al-Lisan (1/241, tafsiri 756) zote katika tafsiri ya Ahmed bin Isa Al-Hashimi. Daraqutni amesema: Msema urongo[.

- Imekuja katika Kanz al-Ummal ya Anas, ambaye amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), amesema: متى ألقى أصحابي؟ متى ألقى أحبابي؟ **“Lini nitakutana na maswahaba zangu? Lini nitakutana na vipenzi vyangu?”**, Baadhi ya Maswahaba wakauliza: Je, sisi si vipenzi vyako? Akasema: أنتم أصحابي، ولكن أحبابي قوم لم يروني وآمنوا بي أنا إليهم بالأشواق **“Nyinyi ni maswahaba zangu, lakini vipenzi vyangu ni watu ambao hawakuniona lakini wameniamini, natamani kuwa nao”** (Abu Sheikh katika ujira). Na imekuja katika Al-Firdaws kwa kauli ya Al-Khattab ya Al-Daylami kutoka kwa Anas bin Malik: مَتى أَلْقى أَصْحَابِي مَتى أَلْقى أحبابي **“Lini nitakutana na maswahaba zangu? Lini nitakutana na vipenzi vyangu.”** Baadhi ya maswahaba wakauliza: Je, sisi si vipenzi vyako? Akasema: أَنْتُم أَصْحَابِي غير أَن أحبابي قوم لم يروني وآمنوا بِي أَنا إِلَيْهِم بالأشواق **“Nyinyi ni maswahaba zangu, lakini vipenzi vyangu ni watu ambao hawakuniona lakini wameniamini, natamani kuwa nao”.** Na Al-Qushayri ametaja katika barua kwa silsila ya wapokezi: Ali bin Ahmed Al-Ahwazi, Mwenyezi Mungu amrehemu, alitwambia: amesema: Ahmed bin Ubaid Al-Basri alitwambia, amesema: Yahya bin Muhammad Al-Jiani alitwambia, amesema: Othman bin Abdullah Al-Qurashi alitwambia , kutoka kwa Naim bin Salem, kutoka kwa Anas bin Malik, amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: متى ألقى أحبابي؟ **“Lini nitakutana na vipenzi vyangu?”** Maswahaba zake wakauliza: Kwa jina la baba yetu na mama yetu, je sisi si vipenzi vyako? Akasema: أنتم أصحابي، أحبابي: قوم لم يروني، وآمنوا بي، وأنا إليهم بالأشواق أكثر **“Nyinyi ni maswahaba zangu, vipenzi vyangu: ni watu ambao hawakuniona lakini wameniamini, natamani sana kuwa nao”.** Hadith hii ina wapokezi wasio tegemewa, na baadhi ya watafiti wamesema kuwa ni hadith ya kukataliwa na ya urongo, ikimaanisha kwamba hadith hii si miongoni mwa hadith zinazokubaliwa zinazotumiwa kama dalili.

4- Hivyo, inakuwa wazi kuwa matni husika si Hadith ya Mtume (saw) bali ni matni changamano, iliyo undwa kwa dhahiri na mtu asiyejulikana na ambamo aliunganisha maneno na maumbo yaliyokuja katika hadith tofauti, ambazo baadhi yake zinakubalika kama dalili, na nyengine ambazo hazikubaliki na hazitumiwi, na kwa hivyo sio sahihi kusimulia. Hivyo basi, si sahihi kusimulia matni inayozungumziwa kuwa ni Hadith kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw). Mwenyezi Mungu ni Mwenye hekima zaidi.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**20 Rabi' al-Awwal 1444 H**
**Sawia na Oktoba 16, 2022 M**


Pepe: info@uqab.or.ke